


TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)



TAARIFA KWA UMMA

UTARATIBU KATIKA AWAMU YA NNE YA UDAHILI KWA MWAKA WA MASOMO 2019/2020

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inatangaza kuwa awamu ya nne ambayo ndio ya mwisho ya udahili kwa mwaka wa masomo 2019/2020 imeanza **Oktoba 01 na itafungwa Oktoba 04, 2019**. Tume inasisitiza kuwa waombaji ambao bado hawajapata vyuo watumie fursa hii vizuri ili kupata nafasi ya udahili.

Tume inasisitiza kuwa waombaji wote waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja na hawajajithibitisha watumie fursa hii kuendelea kujithibitisha katika vyuo wanavyovipenda hadi **tarehe 04 Oktoba, 2019 saa sita usiku**.

Aidha, Tume inaelekeza waombaji na vyuo kuzingatia utaratibu wa udahili kwa awamu ya nne kama unavyooneshwa kwenye jedwali.

Jedwali: Utaratibu wa Udahili katika Awamu ya Nne

Awamu	Muda	Tukio
1.	01 – 04 Oktoba, 2019	<ul style="list-style-type: none">- Kutuma maombi ya udahili awamu ya nne.- Kujithibitisha udahili kwa wale walioshindwa kujithibitisha katika awamu

Awamu	Muda	Tukio
		ya kwanza, awamu ya pili na awamu ya tatu kutokana na sababu mbalimbali.
2.	07- 09 Oktoba, 2019	- Vyuo kuwasilisha Tume majina ya waliochaguliwa katika awamu ya nne ya udahili
3.	09 Oktoba, 2019	- Tarehe ya mwisho ya Vyuo kuwasilisha majina ya waliodahiliwa katika awamu ya nne ya udahili.
4.	10 Oktoba, 2019	- Tarehe ya kutangaza majina ya waliodahiliwa katika awamu ya nne ya udahili.
5.	10 - 13 Oktoba, 2019	- Kujithibitisha udahili kwa waombaji waliochaguliwa zaidi ya chuo kimoja katika awamu ya nne ya udahili pamoja na wale walioshindwa kujithibitisha katika awamu zilizopita kutokana na sababu mbambali.

Waombaji wote wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusiana na udahili au kujithibitisha yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika na siyo TCU.

Imetolewa na:

Prof. Charles D. Kihampa,
Katibu Mtendaji,
TUme ya Vyuo Vikuu Tanzania,
 02/10/2019.